

*Nauli za Mizigo katika Ziwa Victoria*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA 625 la tarehe 01/09/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,  
(SURA YA 415)

---

**AMRI**

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

AMRI YA NAULI ZA MIZIGO KATIKA ZIWA VICTORIA YA MWAKA 2023

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

- |  |  |
|--|--|
| Jina na<br>tarehe ya<br>kuanza<br>kutumika | <b>1.</b> Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Mizigo<br>Katika Ziwa Victoria ya Mwaka 2023 na itaanza kutumika baada ya<br>siku kumi na nne tangu tarehe ya kuchapishwa.  |
| Matumizi                                   | <b>2.</b> Amri hii itatumwiwa na meli zinazomilikiwa na Kampuni<br>wakati wa kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo maeneo ya<br>Tanzania katika Ziwa Victoria.  |
| Tafsiri<br><br>Sura ya<br>415              | <b>3.</b> Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji<br>vinginevyo-<br>“Sheria” maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;<br>“Kampuni” maana yake ni Kampuni ya Huduma za Meli<br>iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni; |
| Sura ya<br>212                             | “Shirika” maana yake Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania<br>lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;<br>“meli” maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika<br>Ziwa Victoria.  |

*Nauli za Mizigo katika Ziwa Victoria*

*TANGAZO LA SERIKALI NA. 625 (Linaendelea)*

**SEHEMU YA PILI  
NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA**

Nauli  
zilizoidhini  
shwa

Sura ya  
165

Masharti  
ya huduma

Sura ya  
165

**4. Kampuni inayoendesha meli: -**

- (a) itatoza nauli ya mzigzo isiyozidi ongezeko la asilimia 17.7 kutoka kiwango cha nauli ya mzigzo kilichoidhinishwa kwa njia ya Mwanza-Bukoba;
- (b) itatoza nauli ya mzigzo isiyozidi ongezeko la asilimia 16.9 kutoka kiwango cha nauli ya mzigzo kilichoidhinishwa kwa njia ya Mwanza-Ukerewe;
- (c) itatunza taarifa za usafirishaji abiria na mizigo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo udhibiti;
- (d) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini.

**5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:**

- (a) itatengeneza chati za nauli za mizigo kwa kuzingatia masharti ya aya ya 4(a) na (b) na kuwasilisha chati hizo kwa Shirika ndani ya siku saba tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;
- (b) itatoa tiketi kwa abiria zinazoonesha nauli isiyozidi viwango vilivyooidhinishwa;
- (c) itatoa tiketi kwa abiria wakiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;
- (d) itapima uzito wa mizigo ikiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;
- (e) itaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuongeza idadi ya abiria na shehena;
- (f) itazingatia ratiba ya safari za meli kama ilivyotolewa na Kampuni kwa wateja; na
- (g) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.

Dar es Salaam  
1 Agosti, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE  
*Mkurugenzi Mkuu*